**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU -**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SABASABINI

**July, 2026**

**Ushetu-Kahama**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**MKOA WA SHINYANGA**

**SHULE YA SEKONDARI SABASABINI,**
**S.L.P 50**
**USHETU-KAHAMA.**
**July, 2026**

**MAWASILIANO YA SIMU**

- **Mkuu wa Shule**:
  0754362637
- **Makamu Mkuu wa Shule;**
  0767591624/0624807759
- **Patron**
  0622398056

*Unapojibu tafadhali taja kumb Na : UDC/SBSB/S.4940/2026*

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SABASABINI, HALMASHAURI YA USHETU MKOA WA SHINYANGA MWAKA.............................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Sabasabini ipo umbali wa Kilometa 37 Magharibi mwa Mji wa Kahama mwelekeo wa barabara ya kahama-Bulungwa, shule ipo mkono wa kushoto umbali kidogo kabla ya kufika senta ya **sabasabini**, usafiri wa basi kutoka kahama mjini unapatikana katika

kituo kidogo cha mabasi **'STENDI YA DODOMA'** nauli ni shilingi **5,000/=** kwa hice na shilingi 10,000/ = kwa pikipiki. Muhula wa Masomo unaanza tarehe kadri utakavyotangaziwa na serikali, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe tajwa. Mwisho wa kuripoti ni tarehe tajwa.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali 02 ambapo moja ni ya rangi ya darkblue (Creta) na suruali ya pili ni ya rangi ya ugoro.(Ili kuepuka kubadilika kwa rangi ya kitambaa angalia kabla ya kurudufisha).Pia zinapatikana kwenye duka la shule.

ii. Mashati 02 meupe yenye mikono mirefu.

iii. Tai ndefu 02 za rangi ya dark blue.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba.

v. Soksi nyeusi.

vi. Sare za michezo ni bukta na tisheti yake, (zote ziwe rangi ya blue) pamoja na raba nyeusi.

vii. Sweta moja 01 yenye mikono mirefu ya rangi ya blue bahari yenye shingo ya V.(Pia linapatikana kwenye duka la shule Kwa bei ya 16,000 Kwa wale ambao watahitaji)

viii. Nguo za kushindia (shamba dress) 02 track suit ya rangi nyeusi( Zinapatikana kwenye duka la shule).

ix. Tisheti mbili za rangi ya kijivu zenye kola na nembo ya shule.(Pia inapatikana kwenye duka la shule ikiwa na nembo ya shule kwa bei ya Tsh.15,000/= kwa watakaohitaji)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 12

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) aina ya **DOUBLE A** kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology

v. Godoro futi 2.5 au 3

vi. Mashuka pair 2 yenye rangi ya blue, blanket 1, fornya 1, chandarua 1 ya rangi nyeupe

vii. Vyombo vya chakula( sahani ,bakuli , kijiko na kikombe)

viii. Ndoo 2 ndogo na kubwa 1 zenye mifuniko

ix. Vifaa vya usafi

PCB - Jembe , Mopa , Mfagio mlaini (soft broom) na Chelewa

PCM - Jembe , Mopa , Mfagio mlaini (soft broom) na Chelewa

HGL - Jembe , Reki , Kwanja na Mfagio laini(soft broom)

HGK - Kwanja , Mfagio mgumu(hard broom) , Mopa na Chelewa

x. Mwanafunzi anashauriwa kuja na taa ya mwanga wa jua kwa matumizi endapo umeme umekatika
xi. Mfuko au begi dogo la kubebea Madaftari na Vitabu
xii. Vifaa vya kujifunzia darasani kama vile kalamu, madaftari, penseli, mathematical set,non prograннable scientific calculator (fx-99 MS)
xiii. Bima ya Afya

## 2.3 Michango mbalimbali

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 30610016622** jina **SABASABINI SECONDARY SCHOOL** katika benki ya **NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye paying slip).

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa wa Baba, mama, mlezi, kaka, na Dada pekee**).
- **Jukumu la matibabu ni la mzazi/mlezi unashauriwa kumfungulia mwanao bima ya afya akiwa nyumbani.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na


xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu sana katika shule hii**




**YONA Z. MTINDA**
**Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na ;**

- **Mkuu wa shule 0754362637**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0624807759**

## MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by a government medical officer in respect of form Entrants.

Student's full name…………………………………………………………..

Blood count (red and white)………………………………………………..

Stool examination……………………………………………………………

Analysis………………………………………………………………………………..

Syphilis test………………………………………………………………………….

Eye test……………………………………………………………………………….

Ears…………………………………………………………………………………….. 

Chest………………………………………………………………………………….

Spleen…………………………………………………………………………………

Abdomen…………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION:** Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases etc.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

certify that person examined above is fit/unfits for admission into a boarding school.

Signature…………………………………….

Designation…………………………………….

Station……………………………………….

Date…………………………………………

**MAELEZO BAYANA (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. jina kamili la mwanafunzi………………………………………….
2. tarehe ya kuzaliwa………………………………………
3. jina la baba/mlezi………………………………….
4. jina la mama……………………………………...
5. kazi anayofanya baba……………………………
6. kazi anayofanya mama……………………………...
7. anuani ya baba/mama………………………….
8. anakilema chochote…………………………………...
9. anapendelea kushiriki michezo gani?.....................
10. taja ndugu wasiopungua wanne(4) wa karibu wanaoweza kutoa msaada/kumtembelea mwano awapo shuleni pale inapobidi.

| S/NO | JINA | UHUSIANO | KAZI | NO.ZASIMU |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**MAKUBALIANO (IJAZWE NA MWANAFUNZI/MZAZI)**

1. Baada ya kusoma kwa makini maelezo, taratibu za sheria za shule. Mimi mwanafunzi (majina)………………………………………………………….

   sahihi…………………………………..

   naahidi kuwa nitatekeleza kwa vitendo yote yaliyotajwa na kwamba itakuwa kosa kukiuka taratibu kanuni na sheria za shule.
2. mimi (mzazi) ………………………………….. nimesoma sheria na taratibu za shule na nakubaliana nazo na kwamba kama mzazi nitakuwa msitari wa mbele kushirikiana na walimu katika kusimamia malezi, nidhamu na taaluma ya mtoto wangu.

   sahihi……………………………………………………

**SHULE YA SEKONDARI SABASABINI**
**USHETU-KAHAMA**
**SHINYANGA**